TOLEO NO.70

# Khilafah

RAJAB 1447 HIJIRIA — JANUARI 2026 MILADIA ( Bei Tsh 4,000/= - Ksh 200/=)

NDIO SULUHISHO

## MADHILA YA KUANGUSHWA KHILAFAH



Hatimae mwishoni mwa mwezi wa Rajab Mwaka 1342 Hijri (Machi 1924 miladi) Serikali ya Khilafah ya mwisho iliyotawala kwa karne 14 mfululizo iliangushwa (Khilafah Uthmania). Hili lilifanikiwa baada ya mapambano makali ya muda mrefu kutoka kwa maadui wa Uislamu kwa msaada wa vibaraka wao wa kiarabu na kituruki.

Waislamu tumepata pigo kubwa na chungu kwa kuangushwa Khilafah ya mwisho (Khilafah Uthmania) lakini kibaya zaidi ni kuwa makafiri wa kibepari ambao ndio waliopambana vikali mpaka kuiangusha dola kwa msaada mkubwa wa Mustafa Kamal wanaendelea mpaka leo kwa bidii ya hali ya juu usiku haitorejea tena katika uhai.Kuangushwa kwa Khilafah halikuwa tu jambo la msiba kwa Waislamu bali pia ni tukio lililopelekea kusita moja kwa moja utawalishaji wa mfumo kamili wa maisha wa Kiislamu katika nyanja ya kiutawala. Mbali na athari nyingi zilizotokana na kuangushwa kwake. Baadhi ya majanga yanayotusibu ni kama yafutayo:-

1.**Waislamu kutokuwa na athari yoyote kimataifa**: Ulimwengu wa Kiislamu una kila sifa na haki ya kuutingisha ulimwengu. Mfumo wake wa Kiislamu pamoja na utajiri wa rasilimali ya mafuta ungeliifanya dunia kunyenyekea chini ya matakwa yake, mbali na rasilimali nyengine nyingi zilizojaa katika ardhi zake. Kadhalika, utajiri mkubwa wa matrilioni ya dola ambazo nchi za kiarabu huingiza kila leo kama mapato ya bidhaa na biashara ya mafuta ni silaha tosha ya kujenga ushawishi na athari

**Inaendelea Uk. 3**

## UPUNGUFU WA MAJI JIJINI DAR ES SALAAM



Mnamo siku ya Jumapili Desemba 14, 2025, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (Dawasa) ilitoa ratiba ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa jiji hilo. Huku katika baadhi ya maeneo ndoo ya lita 20 ya maji kutoka kwa wauzaji wa mtaani imefikia hadi Sh1,000 mara tano zaidi ya bei ya kawaida.

Tangu uhuru wa bendera, Tanzania na husuaan jiji la Dar es Salaam halijawahi kupata maji ya kudumu. Kwa mfano, mwaka jana 2024, 2022 na 2021 jiji lilikua na uhaba wa maji. Upungufu uliopo hivi sasa kama ilivyoelezwa na serikali umetokana na kushuka kwa kasi kwa kiwango cha uzalishaji katika mtambo wa Ruvu kulikosababishwa na kuchelewa kwa mvua.

Shida ya maji nchini Tanzania ni ya kudumu, karibu kila

**Inaendelea Uk. 6**

## Yaliyomo :


- **Rajab mwezi wa Majonzi na Matumaini ………………2**
- **Nani hukabidhiwa zakat bila ya Khilafah? ……….…….4**
- **Mwaka mpya tukio lisilozingatiwa ipasavyo…………..7**
- **Rajab na muhanga wa wanawake ………………………..8**

# RAJAB: MWEZI WA MAJONZI NA MATUMAINI

Msiba wa kuangushwa Dola ya mwisho ya Kiislamu ya Khilafah Uthmania ulitokea tarehe 28, Rajab 1342 AH sawa na tarehe 03, Machi, 1924. Janga hili ni matokeo ya uvamizi na mashambulizi makali ya kifikra, kisiasa na kijeshi kutoka kwa makafiri. Hila na njama za makafikri ndizo ambazo kwa kiasi kikubwa zilichangia kupatikana mporomoko wa kutisha wa ufahamu thabiti (interlectual decline) kwa Waislamu binafsi na dola yao.

Kufifia na kudorora huko kiufahamu kwa Waislamu pamoja na mambo mengine pia kulichangiwa kudharauliwa kwa lugha ya kiarabu. Jambo lililopelekea kufifia kwa ijtihadi. Aidha, dola nayo ilidhihirisha makosa fulani fulani katika utabikishaji wa Uislamu.

Kuna kipindi hata kabla ya uvamizi wa moja kwa moja wa makafiri Makruseda na Wamongoli, dola ilisitisha zoezi la kufungua miji na kutanua mamlaka yake. Na hata pale lilipondelea, mkazo mkubwa ulikuwa ni kutanua ardhi pekee, bila ya kumakinisha ipasavyo ufahamu thabiti wa Kiislamu kwa Waislamu na raia wasiokuwa Waislamu. Udhaifu huo ulianzia tangu karne ya 5 Hijria na athari za udhaifu huo zilidhihirika wazi wazi mwishoni mwa dola ya Khilafah Uthmania

Njama na mikakati ya madola ya kikafiri kuangusha dola haikuwa ni shambulio la mara moja. Bali ni mikakati ya takriban karne tatu mfululizo. Ikihusisha uvamizi wa kithaqafa (cultural Invasion) kupitia wamishenari. Hilo ni kwa kuasisi vituo vyenye sura ya kidini na guo la kisayansi ndani ya nchi ya Malta karne ya 16, na Biladu-Sham mwaka 1820. Vituo hivyo vilipenyeza fahamu na fikra hatari kama utaifa, uzalendo, umaeneo, umadhehebu nk. ili kujenga msingi wa fikra ya kuasi dola ya Khilafah na kujitenga. Vituo hivyo vilikuwa na malengo ya kuvunja mshikamano wa Waislamu, na kuwatenga waarabu kando kutoka katika dola.

Pia kulitendeka uvamizi wa kisiasa (political Invasion) kwa kuchochea uasi ndani ya sehemu za dola ya Kiislamu. Kwa mfano, Uingereza na Ufaransa waliunga mkono na kuchochea harakati za uasi wa Balkans (nchi za Albania, Bulgari, Boznia, Herzegovia,Croatia, Kosovo, Serbia nk) katika mwaka 1804. Aidha, wakaichochea Ugiriki kuasi mwaka 1821 nk.

Uvamizi wa kijeshi moja kwa moja pia ni mkakati uliotumika. Mwaka 1762-1796 Urusi iliipora Cremia, 1884 wakainyakuwa Turkistan na hatimae kumega maeneo ya Caucas. Mwaka 1798 Ufaransa liivamia Misri, 1799 Al-Sham, 1881 Tunisia, ikafuatia Marrakesh (Morocco) nk. Italia nayo ikaimiliki Tripoli (Libya) mwaka 1911. Uingereza ikanyakuwa Yemen mwaka 1839, Rasi ya Uarabuni (Arabian Peninsula), India, kisha mwaka 1882 iliitwaa Misri na kufuatiwa na Sudani. Uholanzi nayo ikapora Mashariki ya India. Afghanistan na Iran ziliwekwa chini ya kinyang'anyiro cha waingereza na warusi.

Adui mkubwa na silaha nzito ya mwisho ya kumalizia dola ya Khilafah ilikuwa vibaraka na wasaliti miongoni mwa waarabu na waturuki. Nao ni masekula wanaobeba fikra za kizalendo na kuzama katika thaqafa ya kimagharibi. Mfano, Mustafa Kemal Attaturk na wasaliti wa kisiasa kama Sharif Hussain ibn Ali, Ibn Saud nk.

Mizizi ya uzalendo ilipokita, mwaka 1916 Uingereza ilimuamuru kibaraka wake Sharif Husain ibn Ali, aliyekuwa gavana wa Khilafah ndani ya Makka kuanzisha uasi wa waarabu dhidi ya Khilafah. Uasi huo ulifaulu katika kuzigawanya ardhi za waarabu kutoka kuwa chini ya Khilafah na kuwa chini ya Uingereza na Ufaransa.

Hatimae mwaka 1924 ikatangazwa rasmi kuvujwa Khilafah ambayo hatunayo hadi leo.

Japo Rajab ni mwezi wa majonzi na huzuni kubwa kwa tukio la kuangushwa dola ya Khilafah Lakini kwa upande wa pili ni mwezi wa bishara na matumaini kwa kuwa tumepewa bishara ya kurudi tena dola hiyo.

Hata hivyo, ni wajibu Waislamu waamshe hisia na nishati mpya ndani ya nyoyo zao kwa kuufanyia kazi Uislamu kwa ulinganizi ili urudi tena katika kiwango cha kiutawala kama ulivyoletwa, na kama ulivyobebwa na waliotutangulia.

**Mhariri**

**Rajab 1447 Hijria**

**Januari 2026 M**

***jukwalakhilafah@gmail.com***

*******************

## Majanga kwa Kuangushwa Khilafah... *kutoka uk .1*

kimataifa. lau tungekuwa na Khilafah. Zaidi ya hayo madhila ya Gaza na Palestina kwa jumla yangeondoshwa kwa nguvu zote. Aidha, rasilmali hizo za Umma zingekuwa ni shinikizo tosha la kuwatoa askari wavamizi wanaoongozwa na Marekani waliosheheni ndani ya miji tofauti ya Kiislamu. Kama vile Iraq, Afghanistan, Somalia nk. Bali kutokana na khiyana ya vibaraka wa nchi za Waislamu, fedha za mafuta haya hupewa bure madola ya kikoloni kama tulivyoshuhudia katika ziara ya Trump mwezi Mei 2025 namna alivyovuna katika ziara yake Mashariki ya Kati.

Siku chache kabla ya kutangazwa rasmi kuangushwa Khilafah, gazeti la "The Times' la tarehe 07/03/1924 lilimnukuu mwandishi wake kwa kusema:

***"Uturuki sasa imeshadondoshwa na kuangushwa kutoka kuwa dola yenye ushawishi na athari katika ulimwengu hadi kufikia kuwa dola isiyokuwa na umuhimu wowote katika Balkan".***

Pia Mnamo tarehe 24/07/1924 miezi michache tangu kuangushwa Khilafah, Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza, Lord Curzon wakati akilihutubia Bunge la Uingereza (House of Commons) alisema:

***"Uturuki imeshaanguka na haitanyanyuka tena, kwa sababu tumeivunja nguvu yake ya kiroho, Khilafah na Uislamu".***

Ukweli wa kauli hizi unadhihirika leo baada ya miaka 105(H) toka kuangushwa kwa Serikali ya Khilafah iliyokuwa na makao makuu katika ardhi ya Uturuki ambayo athari na ushawishi wake haukuwa tu katika eneo la Balkan bali ulimwenguni kote.

2. **Kuzigawa ardhi**: Kuangushwa kwa Khilafah kulipelekea kuzigawa ardhi za Waislamu chini ya usimamizi wa makafiri na kuekewa viongozi vibaraka watiifu kwa makafiri na kuundiwa vijidola telee! Ardhi ambayo kwa ukubwa wake kabla ndiyo iliyojenga dola moja kubwa ya Khilafah ambayo tawala zilisalimu amri chini ya nguvu zake ikasambaratishwa. Leo hii imefikia kutokuwa na thamani yoyote na kuwa vijidola vingi na bado ardhi zetu zinaendelea kukatwa vipande vipande, huku tukiwa hatuna bathari yoyote zaidi ya uadui wa kiaswabia unaozaa mizozo ya kipuuzi ya mipaka baina ya Umma wetu.

3.**Kurudi nyuma kiuchumi**: Matatizo kadhaa yanaousibu leo ulimwengu wa Kiislamu likiwemo tatizo kubwa la kuwa nyuma kiuchumi na kiteknologia ni kutokana na vibaraka kuwa wakala wa makafiri na hawana maamuzi yao wenyewe. Zaidi ya hayo, rasilimali kadhaa ikiwemo mafuta, madini kama dhahabu, ardhi bora kwa kilimo yanaziingizia mabilioni ya dola nchi za Kiislamu, lakini bado utashuhudia maelfu ya Waislamu wakiwemo wataalamu muhimu wakizikimbia nchi zao na kuhamia Ulaya kwa kutaraji maisha bora. Utajiri mkubwa wa mafuta na rasilmali watu wakiwemo wasomi katika nchi zetu vingetosha kuufanya ulimwengu wa Kiislamu kusifika kwa viwanda vizito na wa ulimwengu wa nchi zilizoendelea. Lakini bado utakuta nchi hizi hazina zaidi ya vijiwanda vya kuzalisha pipi, ice cream na nguonguo ilhali utajiri wote ukimalizikia katika mifuko ya watawala vibaraka, familia zao na wapambe wao. Bali la kusikitisha zaidi nchi za Kiislamu zinabakia kuwa soko la bidhaa za kigeni zaidi toka nchi za Magharibi kama si jaa kamwe!

4. **Ukosefu wa amani:** Vita dhidi ya ugaidi vimechora picha ya kukosekana amani na kudhihirisha uovu wa vibaraka ndani ya nchi za Kiislamu ambao wako kifua mbele katika ***vita hivi dhidi ya Uislamu*** vinavyoongozwa na Marekani. Bali zaidi nao vibaraka wamekuwa mstari wa mbele katika kuendeleza unyama, mateso na ukandamizaji kwa raia wao hao. Kama yanayojiri leo ndani ya Syria, Yemen, Saudia, Bahrain, Pakistan nk.

Baada ya kuangushwa Khilafah Waislamu hawajashuhudia tena amani ya uhakika. Tunaona uvamizi wa kijeshi wa Marekani moja kwa moja dhidi ya ulimwengu wa Kiislamu, damu inavyomwagika ndani ya Gaza na vibaraka wakibariki mauaji ya maangamizi kwa kila aina ya msaada kwa mayahudi. Mateso ya Waislamu ndani Kashmir, Myanmar, Turkistan ya Mashariki nk . Bila ya kutaja fitna za kimadhehebu na vikundi vya kigaidi vilivyoasisiwa na Marekani kama ISIS ili madola ya magharibi wapate kujihalalishia uingiliaji kati kama Nigeria kwa lengo la kupora rasilmali.

## NANI HUKABIDHIWA ZAKAT KWA KUTOKUWEPO DOLA YA KIISLAMU?

**Swali:**

Katika qadhia ya Zakat, nani ana haki ya kukabidhiwa kwa kukosekana Khilafah? Tunataraji utatupatia ufafanuzi.

**Jawabu:**

Zakat hutekelezwa kama ifuatavyo:

1-Zaka ya dhahabu na fedha (pesa) inafaa kumkabidhi anayehusika na zaka katika Dola nayo (dola) itawafikishia inayowastahikia. Na inajuzu kwa yule mtoaji kuwapa inaowastahikia, nao ni mbea/aina nane zilizotajwa katika Aya Tukufu ***"Hakika ya zaka ni kwa ajili ya mafakiri, masikini, wanaoitendea kazi, wenyekuzoeshwa nyoyo zao, watumwa wanaohitajika kukombolewa, wenye madeni, katika njia ya Allah (Jihadi), na aliyekatikiwa na safari, hiyo ni faradhi kwenu kutoka kwa Allah. Na Allah ni mjuzi na mwenye hekima"***

2-Zaka ya wanyama, mazao (nafaka) na matunda hukabidhiwa muhusika wa zaka katika Dola na yeye ataifikisha kwa wastahikia. Wala haifai kutolewa zaka yake (aina hii) kutoka kwa mtoaji isipokuwa kwa njia ya Dola.

3-Yote haya pindi tu ikiwa Dola ya Khilafah ipo, wakati huo zaka ya wanyama, mazao na matunda itatekelezwa kwa njia ya Dola kama ni wajibu (*wujuuban)* na sio kwa njia ya mtu binafsi mmoja.

Pia zaka ya dhahabu, fedha (pesa) na biashara inafaa kuitoa kwa njia ya Dola au njia ya mwenye nayo moja kwa moja.




4-Ama hivi sasa kwa kuwa hakuna Dola ya Khilafah ambayo inatekeleza ahkam za kisharia, watu binafsi mmoja mmoja watatoa zaka ya mali zao ikiwa za wanyama au mazao au matunda au biashara au dhahabu na fedha, watazitoa watu binafsi kwa kuwapa zinaowastahikia kwa mujibu wa ahkam za sharia na watahakikisha hilo. Na Allah ndie mwenye kuwafikisha.

Yameelezwa yafuatayo katika kitabu cha Al Am-wal, mlango wa zaka kwa Khalifah uk:170: (Hutolewa zaka ikiwa ya wanyama, au mazao, au matunda au pesa, na mali ya biashara kwa kupewa Khalifah au aliye kwa niaba yake miongoni mwa mawali na ma-*amil* au anaowateua katika makarani na wakusanyaji wa zaka. Amesema Allah Mtukufu: ***"Chukua katika mali zao zaka uwatoharishe na uwasafishe kwayo na waombee dua, hakika dua yako ni utulivu kwao"*** *(Tauba: 103).*

Hakika Allah amemuamrisha Mjumbe wake katika Aya hii achukue zaka kwa wenye mali, na alikua Mjumbe (SAAW) akiteua mawali, ma-amil na waandishi wa zaka ili waichukue kutoka kwa wenye mali, kama alivyokua akiwateua wakadiriaji wakadirie mitende na mizabibu. Watu wakati wa Mtume SAAW walikuwa wakimpa yeye zakat au wale anao wateua katika mawali ma-*amil* na makarani wa zaka…

Na zimepokewa riwaya kadhaa kutoka kwa masahaba na matabiina za kujuzisha mtu mwenyewe kugawa zaka na kuziweka katika sehemu zake katika mali zisosema (*asswamitah)* yaani pesa. Hakika amepokea Abu Ubaid kwamba Kaisan alikuja kwa Umar na dirham mia mbili za zaka, na akamwambia: "Ewe Amiir Al-mu-uminuun hii ndio zaka ya mali yangu" Umar akamwambia: "Nenda ukaigawe". Pia amepokea Abu Ubaid kutoka kwa Ibn Abass kauli yake: "Ukiiweka wewe katika sehemu zake na hukumhesabia (hukumpa) chochote kati yake ambao unawasimamia (watu wako wa nyumbani), basi hakuna kosa". Na pia pamepokelewa kutoka kwa Ibrahim na Al-Hassan wamesema: "Iweke sehemu zake na ifiche". Haya ni katika visosema (*asswaamit)* yaani pesa. Ama wanyama, mazao na matunda hapana budi kuzitoa kwa Khalifah au kwa anaowateua. Abu Bakr amepigana vita dhidi ya wanaozuiya zaka wakati walipojizuiya kuitoa kwa mawali na waandishi ambao amewateua. Na akasema: *"Naapa kwa Allah lau watanizuiliya kamba ya kufungia mnyama ambayo wakiitoa (kama zaka) kwa Mjumbe wa Allah (SAAW) basi nitapigana nao vita kwayo".* (Bukhar na Muslim )

**Ndugu yenu Ata Ibn Khalil Abu Rashtah**

**Ramadhan 1438H./ Juni 2017M**

**1.Hijra ya Uhabeshi.**

Mtume (SAAW) aliwaruhusu baadhi ya masahaba kuomba hifadhi ndani ya nchi ya Uhabeshi/ Ethiopia kufuatia mateso ya Maqureish. Waliondoka Waislamu 16 wanaume, na wanawake 2. Akiwemo Uthman bin Affan Ra. na mkewe Bi Ruqayah bint Rasullulah SAAW.

**2.Kufariki kwa bwana Abuu Twalib**

Ami yake Mtume SAAW aliyekuwa ngome iliyokuwa ikimkinga na kumuhami dhidi ya Maqureish alifariki akiwa na umri wa miaka 82 (Tukio hili ama lilitokea katika Rajab au Ramadhan, mwaka wa 10 wa Utume)

**3.Safari ya Israi na Miiraj.**

Hii ilikuwa ni safari ambayo Allah Taala alimpeleka Mtume wake SAAW kimiujiza baada ya kuondokewa na watu nyeti na kumpa nguvu kufuatia upinzani wa Maqureishi. Pia ilikuwa ni kama bishara ya ushindi ambapo mara baada ya kurudi alipewa baayah ya kwanza iliyozaa baaya ya pili iliyopelekea kupata nusra.

**4.Kutumwa kikosi cha Nakhlah.**

Kikosi hiki kilitumwa chini ya uongozi wa Abdallah bin Jahshi Al-Assad na askari 12 wa Muhajiriina kwenda katika mji wa Nakhlah ili kukusanya habari na kuitisha misafara ya Maqureish. Yalitokea mapigano na kuuwawa Amri bin Hadhram. Tukio hili walilitumia Maqureish kueneza




propaganda chafu dhidi ya Uislam. Lakini Allah Taala akavunja uvumi wao. Tukio hili ni miongoni mwa sababu za kutokea Vita vya Badr (Mwaka wa 2AH)

**5.Kutumwa Kikosi cha Wadil-Quraa**

Zaid bin Harithah aliongoza kikosi cha watu 12 kwenda Wadil-Quraa kukusanya taarifa za kijasusi dhidi ya makafiri. Kikosi hicho kikavamiwa na wakaazi wa mji huo, wakauwawa Waislamu 9 na kusalimika 3 akiwemo Zaid mwenyewe. (Mwaka wa 6AH.)

**6. Kutumwa kikosi cha Al-Khabt.**

Mtume SAAW alituma kikosi cha watu 300 chini ya Abuu Ubeida Al-Jarrah ili kuwadhoofisha Maqureish kiuchumi.(Mwaka wa 8 AH.)

**7.Ghazwatu-Tabuuk.**

Mtume SAAW alitoka na jeshi la watu 3000 kwenda Tabuuk kupambana na Warumi na vibaraka wao baada ya vita vya Mutah kutofanikiwa vizuri kulipiza kisasi cha balozi wake Al-Harith bin Umair Al-Azd aliyeuliwa na Shurhabil Al-Ghassan. Khofu na hali ya hewa iliwatisha makafiri na kukimbia. Uongozi wa dola ulikabidhiwa kwa muda kwa Muhammad bin Maslamah Al-Answari au Sibai bin Arfata Al-Ghifariy (kwa masimulizi mengine) ( 9 AH.)

**8.Vita vya Yarmouk.**

Vita hivi vilitokea katika zama za Khilafah ya Umar bin Khattwab.

9. Kufariki dunia kwa Imam Abu Hanifa (R.A), mmoja katika maimamu wakubwa wa madhehebu ya AhluSunnah (15 Rajab 150 Hijria).

**10. Kufariki dunia kwa Imam Shafii (R.A) 14 Rajab 204 Hijria**

11.Kufariki dunia kwa Imam Muslim (R.A) mwanachuoni mkubwa wa Hadithi 24 Rajab 261 Hijria.

12.Kufariki dunia kwa Imam Nawawi (R.A), mwanachuoni mkubwa wa madhehebu ya Kishafii. 14 Rajab 677 Hijria

**13.Ukombozi wa Al-Quds na Sallahudin Ayoub.**

Baada ya Msikiti mtukufu wa Baiutil Muqadas kuwa chini ya Makruseda kwa miaka mingi Waislamu waliweza kuukomboa na kuurejesha tena katika mamlaka yao chini ya kamanda Sallahudin Ayoub (Allah Amrehemu) katika Tarehe 27 Rajab.

14.Kuangushwa kwa Khilafah ya mwisho (Khilafah Uthmania)

Serikali ya mwisho ya Kiislamu ya Khilafah Uthmania iliangushwa na makafiri kwa msaada wa vibaraka wa kituruki na kiarabu. Khalifah wa mwisho wa 101 Abdul Majid II alifungiwa virago vyake pamoja na familia yake na kufukuzwa katika makao makuu Istanbul, Uturuki. Na huu ndio ukawa mwisho wa Khilafah (Tarehe 28 Rajab 1342 AH / Tarehe 3 March 1924 AD)

***********

## NUKUU

Mnamo tarehe 24/07/1924 miezi michache tangu kuangushwa Khilafah, Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza, Lord Curzon wakati akilikhutubia Bunge la Uingereza (House of Commons) alisema:

*"Nukta ya kuzingatia ni kwamba Uturuki imeshaanguka na kamwe haitohuwika tena, kwa sababu tumeshaangamiza nguvu yake ya kiroho: Khilafah na Uislamu".*






## Upungufu wa maji… *kutoka uk .1*

mwaka ikiwa na viwango tofauti vya ukali. Shida hii imeathiri maisha ya watu kutokana na upatikanaji hafifu wa maji na kusababisha maafa katika sehemu nyingi za jiji, gharama kubwa za kununua maji kutoka kwa wachuuzi na wakati mwingine watu wanalazimika kungoja mgao wao wa maji mpaka majira ya nyakati za usiku wa manane.

Ni aibu kwamba, licha ya Tanzania kuwa na vyanzo vingi vya maji, bado inakabiliwa na tatizo la uhaba wa maji mpaka leo. Kuna maziwa makubwa kama Victoria, Tanganyika, na Nyasa, mito mingi ikiwemo Rufiji, Pangani, Wami, Ruvuma, Mara, Kagera, na Gombe, bila kusahau Bahari ya Hindi, chemchem ya maji chini ya ardhi, ardhioevu na maji ya mvua.

Zaidi ya yote, Tanzania inakabiliwa na matatizo mengine yanayoikabili sekta ya maji kama vile uchakavu wa mabomba na uvujaji holela unaosababisha miundombinu ya maji kuwa katika hali mbaya na kusababisha takriban asilimia 37 hadi asilimia 49 ya maji yanayosambazwa kupotea kutokana na uvujaji huo wa ovyo wa maji.

Hii ina maana karibu nusu ya maji yanayosambazwa yanapotea. Laiti maji haya yangeokolewa huenda upatikanaji wa maji ungekuwa bora kuliko hali ya sasa.

Hivi ndivyo serikali za kibepari duniani kote zinavyoamiliana na watu wao, hawajali mambo ya raia hata katika mahitaji msingi ya maisha kama vile hili la maji.

Suala la kutowajibika na kupuuza katika kuwatumikia raia kwa uadilifu liko mbali katika ubepari, kwani msingi wa mfumo huu na nidhamu yake ya kisiasa ni maslahi binafsi tu.

Kwa hiyo, kila mmoja ndani ya mfumo huu kuanzia wanasiasa na watumishi wa Umma kuwa wana ajenda moja tu ya kujitajirisha wao wenyewe, familia zao na wapambe wao na kamwe hawapo kushughulikia matatizo ya wananchi. Ni suala la maslahi binafsi ndiyo yaliyowasukuma wanasiasa kutafuta nyadhifa zao za kisiasa na kamwe siyo shauku ya kutumikia na kutatua matatizo ya watu.

Kinyume chake katika Uislamu, jukumu la serikali ya Khilafah ni kuhudumia watu na kipaumbele chake kikuu ni kuwafanya watu wote wapate mahitaji yote ya kimsingi kwa ajili ya kuishi. Dola ya Kiislamu (Khilafah) inawajibika kutoa huduma zote za kijamii kwa raia wake wote bila malipo au kwa gharama nafuu. Ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii kwa wote, ni marufuku kubinafsisha vyanzo vikuu vya maji au mali nyingine yoyote ya Umma.

**Imeandikwa na:**

**Said Bitomwa**

**Mjumbe wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Tanzania**

**Kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

*****************

Allah Taala kwa Rehma Zake licha ya kuleta Mitume As. kuwaongoza wanadamu namna ya kumuabudu Mola wao na kuwapa sharia kutoka kwa Mola wao kusimamia maisha yao, pia akawawabakishia ndani ya maumbile ya nafsi zao utambuzi wa kimaumbile ambao huwawezesha kutanabahi na kujua kuwepo kwa Muumba huyo.

Utambuzi huo ndio huitwa fitra. Maana ya fitra ni ile hisia ya utambuzi wa ndani isiyopingika kwenye nafsi ya mwanadamu kuhisi kusiko na shaka kuwepo anayemtenza nguvu mwanadamu bila ya ridhaa yake. Mwenye nguvu huyo hutenda ayatakayo kwa mwanadamu bila ya mwanadamu kuweza kudhibiti maamuzi hayo. Huyo ndio Mola, Muumba wa mwanadamu na kila kilichomzunguka. Hisia hii ya kuwepo Muumba huyo anayo kila mwanadamu akipenda asipende. kilichobakia ni kwa mwanadamu kukiri hadharani utambuzi wa Mola huyo na kujisalimisha, au kujisahaulisha mpaka arudi kwa Mola wake kustahiki adhabu.

Ukiangalia kwa makini maisha yote ya mwanadamu tangu kuzaliwa kwake, kuishi kwake duniani na kumalizika umri wake kwa kufariki ni miongoni mwa mambo ambayo kwa kila mwenye fikra iliyosalimika bila ya chuki, taasub wala kasumba humpelekea kwenye utambuzi wa kuwepo Mola wake yaani fitra.

Mwanadamu hakujua lini ata




kuja duniani. Aidha, hajui ataondoka lini. Pia kuondoka kwa walioondoka kabla si kutokana na uzembe. Kwa sababu kama sababu ya kufariki kwa waliotangulia ni uzembe, wapo wazembe wengi ambao bado wanaendelea kuishi. Na lau kama sababu ya wanaoishi duniani leo ni kwa kuwa mahodari, wajanja au kuwa na afya njema, basi walikuwepo mahodari wengi, wajanja na waliokuwa na afya njema lakini leo hawapo wameshafariki.

Hili kwa ufupi ni dhihirisho la kuwa mwanadamu hana khiyari katika kuwa na umri mrefu au mfupi, na wala hana athari katika kuendelea kuishi katika maisha haya au kufariki.
Kwa msingi huo, kuingia kwa mwaka mpya, uwe wa kalenda ya Kiislamu au nyengineyo kinachodhihirika ni kusonga mbele kwa umri wa mwanadamu, kuongezeka maisha yake na pia kurefuka muda wa waliotutangulia makaburini. Jambo hilo kamwe mwanadamu hawezi kabisa kuliingilia wala kujipangia kwa namna yoyote. Kwa hivyo, kwa kuingia mwaka mpya na kwa kuwa mwanadamu hawezi kuliingilia suala hilo, ilitarajiwa mwanadamu atanabahi kwa utambuzi wa kuwepo Muumba wake na kujinyenyekeza kwake na sio kufanya vitendo vya fujo, vurumai na ufuska kwa kisingizio cha ati sherehe za mwaka mpya.

Katika mfumo wa kidemokrasia jambo hili ni lenye kutarajiwa.

Kwa kuwa ni mfumo wa fujo na ujanja wa kukimbilia kwenye matawi/mitagaa badala ya chanzo. Ilikuwa mfumo huu umuoneshe mwanadamu ikiwa umri wake umeongezeka, jee amechangia chochote katika kuongezeka huko? Na kwa kuwa hana mchango katika hilo hana budi amkiri Muumba ambae ndie Mpangaji wa hayo na mengineyo. Na kilichobakia ni kumnyenyekea yeye peke yake. Hii ndilo suala la msingi ambalo hupaswa kulikabili kila mweledi na mwenye fikra angafu.

Uislamu umeuita umri wa uzee ulioambatana na udhaifu wa kutoelewa mambo kuwa ni umri mbaya. Kwa sababu katika umri huo mwanadamu anashindwa hata kutambua katika yale aliyokuwa akiyatambua awali. Hii maana yake hata kama umri wa mwanadamu utakuwa ni miaka kumi na tano, lakini akashindwa kuutumia umri huo kuwa na utambuzi thabiti wa mambo, umri huo pia mwanadamu kaufanya kuwa ni umri mbaya.

Kuingia mwaka mpya chini ya mfumo wa kidemokrasia kumefanywa ni kuzama katika umri mbaya kwa sababu kumefanywa mazingira ya kumkosesha mwanadamu ufahamu thabiti wa kumfungamanisha na Mola wake aliyemuumba.

Masoud Msellem

*************



## RAJAB NA MUHANGA MKUBWA WA WANAWAKE

Matukio makubwa ya kitareekh ndani ya mwezi huu wa Rajab licha ya kutupa mawaidha mengi katika dini yetu, pia yanatukumbusha katika historia ni kwa kiasi gani akinamama, dada na mabinti wa Kiislamu walivyojitolea muhanga mkubwa kwa ajili ya dini ya Mwenyezi Mungu. Walijitolea kwa muhanga wa mali, nguvu na hadi kufikia kutoa uhai wao kwa ajili ya Mola wao.

Kwa kuanzia, tukitupia macho kisa cha Miiraj, safari ya miujiza ya Mtume SAAW iliyofanyika mwezi wa Rajab mwaka mmoja kabla ya kuasisiwa dola ya mwanzo ya Kiislamu mjini Madina, tunaona miongoni mwa mambo aliyokutana nayo Mtume SAAW katika safari hiyo ni kaburi lililokuwa likitoa harufu nzuri ya ajabu ! Alipouliza Mtume SAAW kuhusu kaburi hilo, alielezwa na Jibril As. kwamba lilikuwa ni kaburi la mwanamke msusi katika zama za Firaun aliyeshikilia imani ya tawheed kwa uthabiti na kudhihirisha msimamo wake wa haki mbele ya Fir-aun. Fir-aun akaamua kuwauwa watoto wa msusi huyo ili kumshinikiza asalimu amri ya kurudi katika ukafiri. Lakini msusi huyo alisimama kidete bila ya kutetereka hadi Fir-aun akamuuwa na yeye, na mama huyo kufa kifo cha shahid. Muhanga huu wa aina yake ni kwa ajili ya kumpwekesha Mola, Muumba wa ulimwengu.

Aidha, ni katika mwezi huu wa Rajab, ndani ya mwaka wa tano wa Utume ndio mwezi uliofa




nyika tukio la Hijra ya Uhabeshi. Ilikuwa ni kuhama Waislamu kwa ajili ya kukimbia mateso na vitimbwi vya maqureish. Kati ya Waislamu kumi na mbili waliokuwemo katika safari hii, wanne walikuwa wanawake. Waislamu hao walisafiri masafa marefu baharini kwa ajili ya Uislamu wao. Wanawake waliokuwemo katika msafara huu ni Ruqayyah bint Muhammad (binti wa Mtume SAAW, na mke wa Uthman bin Affan, Sahla bint Suhail, Umm Salama na Layla Bint Abi Asmah. Safari hii ya mwanzo ilisahilisha kutokea safari ya pili ya Waislamu kuja Uhabeshi ambayo ilijumuisha Waislamu wengi zaidi chini ya Jaafar bin Abu Talib (ra)

Kwa upande mwengine tusisahau pia ni katika mwezi wa Rajab mwaka wa tisa Hijria ndipo vilipotokea vita vikubwa na vikali vya Tabuk. Vita vilivyokua mtihani mkubwa kwa Waislamu. Kwa kuwa vilitokea kipindi cha kiangazi, kwenda eneo la mbali, kukabiliana na jeshi kubwa la waroma na isitoshe maandalizi yake hayakua na vifaa vya kutosha. Vita ambavyo Mwenyezi Mungu mwenyewe kavipa jina ndani ya Quran kwamba ni 'saa nzito' (saatu l-usra). Waislamu walitakiwa wachangie kadiri wawezavyo katika maandalizi ya jeshi. Ni katika hali kama hiyo ndipo akinamama na mabanati wa Kiislamu walipochangia vito, mikufu, bangili, herini, mapambo yao na vitu mbalimbali vya thamani ili kusaidia katika upatikanaji wa vifaa vya vita.

Imepokewa kutoka Umm Sinan, mwanamke wa kabila la Aslam kwamba aliona pande la kitambaa mbele ya Mtume SAAW katika nyumba ya Aisha ra. ambacho ndani yake kilisheheni vito na vitu mbalimbali walivyochangia wanawake wa Kiislamu ili kusaidia kukabiliana na gharama za maandalizi ya jeshi la Tabuk (Waqidi, Maghazi, Vol. 3, p. 991-992)

Leo muhanga wa wanawake unahitajika kuliko wakati wowote. Kwa sababu tunapita katika kipindi ambacho Waislamu hatuna kinga ya kulinda maisha yetu, heshima yetu, mali zetu na dini yetu, yaani dola ya Kiislamu ya Khilafah baada ya kuangushwa na makafiri mwezi kama huu wa Rajab 1342 Hijri (Machi 1924 miladi) Basi ni wajibu mama zetu, dada zetu warejee katika msimamo wa kitareekh wa kujitolea muhanga kwa ajili ya kuirejesha tena dola ya Khilafah Rashidah.

